# Neno La Mungu

**na**

**Ellis P. Forsman**

# Neno La Mungu

**na**

**Ellis P. Forsman**

**Oktoba 15, 2011**

# Neno La Mungu

## Ebr. 4:12

Moja ya nguvu kuu katika ulimwengu mara nyingi hutazamwa kwa dharau.

Unapofiria kuhusu nguvu kuu katika ulimwengu, mwana damu anafikiria kuhusu mabomu, silaha nzito nzito, au milipuko.

Biblia inasema neno la Mungu lina nguvu.

Ebr. 4:12, "*Maana neno la Mungu li hai tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*"

Katika somo hili tutajifunza mambo matatu ni kwa nini neno la Mungu lina nguvu.

## Neno la Mungu li "hai"

Watu wengi wanatazama Biblia kama kitabu cha kusoma au hadithi.

### Neno la Mungu linajithibitisha lenyewe kuwa li hai

- Yoh. 1:1-3, "*Hapo mwanzo kulikuwako neno, naye neno alikuwako kwa Mungu, naye neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo, wala pasipo yeye hakukufanyika cho chote kilichofanyika.*"

- Yoh. 1:14-17, "*Naye neno <u>alifanyika mwili</u> akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli. Yohana alimshuhudia akapaza sauti yake akasema, huyu ndiye niliyenena habari zake ya kwamba, ajaye nyuma yangu amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu. Kwa kuwa katika utimilifu wake sisi sote tulipokea na neema juu ya neema. Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Mungu; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo.*"

**Hata vitu vilivyo vya maana vilimtii.**

Rum. 6:11, "*Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi <u>na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu.</u>*"

Neno la Mungu husukuma mioyo ili ibadilike; hutia changamoto maisha ya watu katika utumishi; na hushughulikia matatizo ya watu yaliyo magumu – dhambi.

Hivyo basi, neno la Mungu li hai kwa sababu inabadilisha maisha yetu.

## Neno la Mungu "linanguvu"

**Neno la Mungu linafananishwa na mbegu.**

Luka 8:4-15, "*Mkutano mkuu ulipo kutanika, na wale waliotoka kila mji wakimwijia, alisema kwa mfano; mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake; naye alipokuwa akizipanda, nyingine zilianguka karibu na njia, zikakanyagwa, ndege wa angani wakazila. Nyingine zikaanguka penye mwamba, zilipoanza kumea zikakauka kwa kukosa rutuba. Nyingine zikaanguka kati ya miiba, na miiba ikamea pamoja nazo ikazisonga. Nyingine zikaanguka penye udongo mzuri, zikamea zikazaa moja kwa mia. Alipokuwa akinena hayo alipaza sauti akisema, Mwenye masikio ya kusikilia, na asikie. Wanafunzi wake wakamwuliza, maana yake ni nini mfano huo? Akasema ninyi mmepewa kuzijua siri za ufalme wa Mungu, bali wengine kwa mifano, ili wakiona wasione, na wakisikia wasielewe. Na huo mfano maana yake ni hii; mbegu ni neno la Mungu. Wale wa karibu na njia ndio wasikiao, kisha huja ibilisi akaliondoa hilo neno mioyoni mwao, wasije wakaamini na kuokoka. Na wale penye mwamba ndio wale ambao wasikiapo hulipokea lile neno kwa furaha; nao hawana mizizi, huamini kitambo kidogo, na wakati wa kujaribiwa hujitenga. Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lo lote. Na zile penye udongo mzuri, ndio wale ambao kwa unyofu na wema wa mioyo yao hulisikia neno, na kulishika; kisha huzaa matunda kwa kuvumilia.*"

**Mbegu haiwezi kufanya vyema isipokuwa ikipandwa katika moyo ambapo itakuwa.**

Yoh. 6:63, "*Roho ndiyo itiayo uzima mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho tena ni uzima.*"

## Neno la Mungu ni "kali"

**Neno la Mungu linalinganishwa na upanga mkali.**

Ebr. 4:12, "*Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*"

Ukali wake huifanya kuwa imara.

Katika kazi za karakana, mtu anaweza kufanya kosa anapotumia upanga ambao ni butu. Kazi inakuwa rahisi mtu anapotumia kifaa kikali.

Maisha yetu yanaweza kufanya kazi kwa urahisi yanaponolewa na neno la Mungu lililo kali.

**Ili maisha yetu yawe kamilifu ni lazima tuendelee kutumia kifaa cha Mungu kilicho kikali ili kuweza kulainisha sehemu ambazo zimepinda**.

2 Tim. 2:15, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*"

**Neno la Mungu hukamilisha mahitaji yetu yote.**

- 2 Tim. 3:16-17, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"
- 2 Pet. 1:3, "*Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.*"

# Neno la Mungu "lachoma"

Upanga ambao hauna makali haiwezi kutimiza makusudi yake. Haiwezi kupenya.

**Neno la Mungu laweza kuchoma hadi kufikia hatua ya kugawanya nafsi na roho.**

Ebr. 4:12, "*Maana neno la Mungu li hai tena lina nguvu kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, , tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*"

Hutenganisha ukweli kutoka katika uongo.

**Hakuna kinachoweza kufichwa.**

- 2 Kor. 4:1-2, "*Kwa sababu hiyo kwa kuwa tunahuduma hii kwa jinsi tulivyopata rehema, hatulegei; lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uongo; bali kwa kudhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu.*"

- 1 Yoh. 3:20-22, "*Ikiwa mioyo yetu inatuhukumu, kwa maana Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu naye anajua yote. Wapenzi, mioyo yetu isipotuhukumu, tuna ujasiri kwa Mungu; na lo lote tuombalo, twalipokea kwake, kwa kuwa twazishika amri zake, na kuyatenda yapendezayo machoni pake.*"

**Neno huenda sehemu ambapo mwanadamu hawezi kufika au kufikiria.**

1 Kor. 1:25, "*Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu.*"

## Neno la Mungu "hutambua"

Ebr. 4:12, "*Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.*"

Neno la Mungu lina nguvu sana kwamba huweza kutambua mawazo yetu.

Hata tunachokusudia moyoni Mungu anakifahamu. Neno hupata utu wa ndani.

**Hekima ya mwanadamu ni kipofu. Shetani anatudanganya**.

Efe. 6:11, "*Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzishinda hila za shetani.*"

Neno la Mungu huaribu mitego na silaha za shetani.

## Neno la Mungu ni la "milele"

Mat. 24:35, "*Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe.*"

**Dunia na yote yanayoendelea ndani yake yata chomwa.**

2 Pet. 3:10, "*Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.*"

**Tutahukumiwa kwa neno la Mungu.**

Yoh. 12:48, "*Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena litamhukumu siku ya mwisho.*"

Neno la Mungu linatuambia kuhusu Yesu Kristo na jinsi utii wetu kwake unaweza kutupatia uzima wa milele.

# Hitimisho

Mambo haya sita hufanya neno la Mungu kuwa na nguvu.

Je umelitii neno? Wewe ni Mkristo, unayeishi kulingana na neno?

Yafuatayo ni hatua muhimu yanayoweza kufanya hilo liwezekane:

- **Imani**. Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa katika shule ya sekondari (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na wa kwangu akaniambia kwamba alikuwa hamwamini Mungu, kwa vile nilikuwa nimebatizwa nilichukua nafasi kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaona kuwa kuishi maisha ya Ukrsto ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kama Mungu yupo. Lakini ili awe sehemu salama labda anapaswa kwenda kanisani, na siku akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba alihudhuria kanisani na kuishi maisha mema kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na sio motoni (kama kuna moto). Nikamwambia "hayaendi hivyo. Unapaswa umwamini kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba**. Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Mdo. 11:18, "*…Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima</u>.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, na unafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani ya nyumba hii!" hivyo unachukua simu ya mkononi, taratibu unawapigia polisi, ukiwaambia kwamba kuna mwizi ndani kwako, na unawapa anwani yako. Muda kidogo unawasikia polisi wamefika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "Samahani, Samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na sio kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataibatena na kwamba anataka kubadili maisha yake ili kwamba asiibe tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloongoza katika badiliko la tendo. tunapaswa kufanya hivyo kabla hatujafanyika Wakristo.

- **Kiri.** Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Maana kwa moyo mtu <u>huamini</u>*

*hata kupata haki na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

Kumbuka andiko hilo hapo juu kwamba (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekea katika kutu fulani; sio kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ambapo haki, uzima, na wokovu hupatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikasema, huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninaye pendezwa naye.*" (Mat. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema kwamba ni kitu sahihi kufanya. Unaona jinsi Mungu alivyopendezwa wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Ndivyo **itupasavyo** kuitimiza haki yote.*" Tunabatizwa kwa sababu inatiza haki yake, na sio kwa sababu ya haki yetu.

  Hakika, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu".* Kwa nini mtu aache atua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

  Yesu aliagiza kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*"

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*" (Mdo. 22:16). Ubatizo ni hitaji ambalo Mungu ametupatia.

  Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Rum. 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo*

*alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, viyvo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; tukijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike tusitumikie dhambi tena;*" (Rum. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumika katika damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za kale pale tu tunapo batizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza". Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili makaburini na kuuwekea udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama haujafanyika Mkristo, kwa nini usifanyike leo.